



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAJI

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA  
MAZINGIRA MOSHI**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi inawatangazia wananchi wote kwamba itaendesha kwa njia ya mnada wa hadhara uuzwaji wa magari, pikipiki pamoja na vifaa mchanganyiko chakavu siku ya Ijumaa tarehe 20 Mei, 2022 kwenye eneo la kuegesha magari lililoko ndani ya ofisi za Mamlaka.

Mnada huo utahusisha vitu vifuatavyo:-

**MALI ZITAKAZOUZWA KWA NJIA YA MNADA**

NA.	MALI	IDADI
1	Magari	2
2	Pikipiki	13
3	Vifaa vya umeme	2
4	Vifaa vya maji	467
5	Vipuri vya magari	9

**MASHARTI YA MNANDA**

- Chombo /kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo
- Kwa vifaa na samani mnunuzi atalazimika kulipia papo hapo amana ya asilimia mia moja (100%) ya thamani ya kifaa au samani atakayonunua na kuondoa kifaa/vifaa siku hiyo hiyo ya mnada, mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kifaa/vifaa husika.

3. Kwa vyombo vya moto, mnunuzi atalazimika kulipa hapohapo amana ('**Deposit**' isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya chombo alichonunua na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo husika na amana iliyolipwa haitarudishwa.
4. Kwa vyombo vya moto, mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuaanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Mtu yejote atakayetamka bei juu kisha akashindwa kulipa atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.
6. Gharama za kubadilisha umiliki kwa vyombo vya moto ni jukumu la mnunuzi mwenyewe.
7. Ruhusa ya kuangalia vyombo na vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika.
8. Mnada utaanza saa nne kamili (4:00) asubuhi.

***Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki katika mnada huu wa hadhara.***

***IMETOLEWA NA:***

Mkurugenzi Mtendaji

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi

S. L. P. 1001

**MOSHI**